**SHULE YA SEKONDARI SENGEREMA**
**KAZI YA NYUMBANI – LIKIZO YA DECEMBER 2024**
**KIDATO CHA SITA**
**KISWAHILI**

## MAELEZO
:

- Fanya maswali yote katika daftali lako la mazoezi

1. Andika hadithi fupi juu ya ajira kwa watoto, kisha bainisha muundo na mtindo uliotumia.
2. Eleza kwa kutoa mifano ni namna gani utata unaweza kuondolewa kaika mawasiliano.
3. Jadili aina, sifa na umuhimu wa kutumia misimu katika lugha.
4. Jadili utakavyoondoa changamoto za kutumia misimu katika lugha.
5. Tumia mifano kufafanua mambo matano yanayomwongoza mtu katika kuteua maneno, misemo na miundo wakati wa kuzungumza.
6. Kwa kutumia mifano eleza maana na matumizi ya istilahi zifuatazo.
   i. Viambishi
   ii. Mofu changamano
   iii. Mofimu tegemezi
   iv. Upatanisho wa kisarufi.

7 Bainisha dhima ya kisarufi na kimatumizi ya kipashio **’’ji’’** katika sentensi zifuaatazo ;
   i. Haifai kukaa penye vumbi jin<u>gi</u>
   ii. Uchafua<u>ji</u> wa mazingira huleta madhara mengi .
   iii. Asubuhi yake ali<u>ji</u>sikia amechoka sana
   iv. Ujambazi umelizalilisha <u>ji</u>ji letu la amani.
   v. Mimi si msema<u>ji</u> wa shirika letu.

8 Fafanua dhima tano za rejesta katika matumizi ya lugha .

9 Eleza tofauti ya uainishaji wa ngeli kwa mtazamo wa kimapokeo au ule wa kisasa.

10 Jadili mazingira matano ya upokeaji wa umbo la o-rejeshi katika ngeli za nomino.

11 Kwa kutumia mifano onesha tofauti nne (4) baina ya silabi na mofimu. .

12 Tunga sentensi kumi (10) zenye o-rejeshi,kisha chaagua sentensi tano ubainishe aina ya urejeshi uliyotumika.

13 Kwa kutumia mifano eleza maana ya stilahi zifuatazo;
   i. Alofoni
   ii. Alomofu
   iii. Fonimu
   iv. Mofu
   v. Nomino.

14 . ( a) Onesha tofauti iliyopo baina ya mzizi na shina la neno

( b) Eleza zana ya mzizi wa neno kwa kutumia mifano mitano

15 Eleza jinsi biashara na dini zilivyosaidia katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanganyika kabla ya uhuru .

16 Fafanua sababu tano zilizokifanya Kiswahili kifae kuwa lugha ya kufundishia katika viwango vyote vya elimu nchini Tanzania.

17 (a) Weka nomino zifuatazo kwa mtazamo wa ngeli za wanasarufi wa kimapokeo na wa kisasa

i. Mtu
ii. Kipofu
iii. Kijiko

(b) Kutokana na uainishaji wako ,ni upi uainishaji mzuri wa nomino hizo hapo juu (a) katika ngeli ? Toa sababu nne .

18. Mwandikie baba yako barua anayeishi Korogwe S.L.P. 400, ukimfahamisha mahitaji unaayotakiwa uwe nayo ili ushiriki sherehe ya kuhitimu kidato cha sita 2025. Jina lako liwe Martini Marefu S.L.P 42 Sengerema.

19. Kwa kutumia hoja tano madhubuti, jadili kwanini watanzania wengi walio mahiri wa lugha, ubingwa wao husshindwa kupea sawasawa katika lugha hizo wanazo zitumia.

20. Je, utachukua hatua zipi kutunza na kuongeza umahiri wako katika lugha unazozijua? Eleza huku ukitoa mifano dhahiri kwa hoja tano.

21. Eleza dhana ya fasihi kama ilivyojadiliwa na wanafasihi mbalimbali.

22. Eleza tofauti kati ya fasihi na vipengele vingine vya sanaa.

23. Jadili mitazamo kuhusu chimbuko la fasihi kwa kuzingatia ubora na udhaifu wa kila mtazamo.

24. Fasihi ina umuhimu gani katika maisha ya mwanadamu?

25.Kwa kutumia mifano, jadili kauli kwamba “fasihi hubadilika kulingana na jamii inavyobadilika’. Toa hoja tano.

26. Kwa kutumia mifano, fafanua jinsi uhuru wa mtunzi wa kazi za fasihi unavyoweza kuhusishwa na utamaduni wa jamii.

27. Uhuru wa mwandishi wa fasihi ni wa kitabaka zaidi kuliko wa mtu binafsi. Fafanua kwa mifano ukitoa hoja tano.

28. Fafanua dhana ya udhamini wa kazi za fasihi .

29. Udhamini wa ushawishi ni sawa na udhamini wa nnguvu.Jadili kauli hii.

30.Fafanua athari za udhamini wa kazi za fasihi kwa jamii.

31. Eleza ni kwa namna gani jamii nzima ni mdhamini wa kazi ya fasihi. Toa mifano muafaka.

32. Eleza dhima chanya na hasi za fasihi.

33. Nini maana ya hadithi?

34. Fafanua angalau mambo manne yanayoweza kumwongoza mtu kutunga hadithi.

35. Tunga hadithi fupi ya kukanya tabia mbovu katika jamii.

36.Fafanua tanzu hizi za hadithi;

i. Ngano.
ii. Tarihi
iii. Visasili
iv. Vigano.
v. Soga
vi. Visasili.

37. Fafanua maana yaa semi.

38. Methali hubeba dhima mahususi, tumia methali angalau tano kati ya ushairi na utenzi.

39. Tamthiliya ni sawa kabisa na sanaa za maonesho.Fafanua kauli hii kwa mifano mitano.

40. Jadili athari za utani unaofanyika katikaa jamii ya Watanzania.

41. Kwa kutumia mifano isiyopungua mitano, eleza tofautti zilizopo baina ya Tamthiliya na Riwaya.

42. Tumia watunzi wawili wa tamthiliya ulizosoma ukionesha ni namna gani wametofautiana kimuundo wa tamthiliya zao.Tumia hoja tatu kwa kila mtunzi.

43.Eleza angalau mitindo minne iliyojitokeza katika tamthiliya mbili ulizosoma.

44. Hitimisho la migogoro katika Riwaya huijenga jamii upya. Tumia hoja nne kwa kila riwaya ukifafanua kauli hii.

45. Tumia watunzi wawili wa Riwaya ulizosoma ukifafanua hoja nne kwa kila mmoja kuhusu kufaulu na kutofaulu kwao katika utunzi wa Riwaya zao.

46. Matumizi ya lugha ndio huiwezesha jamii ipokeayo kazi ya fassihi kutanabaisha maudhui ya kazi hiyo. Tumia Riwaya mbili ulizosoma kudhihirisha kauli hii ukitoa hoja angalau nne kwa kila riwaya.

47. Watunzi wengi wa Tamthiliya hutoa ujumbe Fulani ili kusisitiza au kukosoa mambo kadhaa katika jamii zao. Tumia watunzi wa Tamthiliya mbili ulizosoma kudhihirisha suala hili.

48. Kwa kutumia mifano, Fafanua mambo ya kuzingatia katika usanifu wa maandishi.

49.Eleza maana ya vipera hivi vya semi;

i. Methali
ii. Misemo
iii. Nahau
iv. Mizungu
v. Mafumbo
vi. Lakabu
vii. Misimu
viii. Vitendawili.

50. Watunzi hutumia miundo na mitindo katika kutoa uumbaji wa kazi zao. Eleza miundo miwili na mitundo miwili iliyotumiwa na kila mtunzi katika uumbaji wa kazi yake. Tumia riwaya mbili ulizosoma.